

## Mathayo 20 : 29 - 34

Wakati Yesu anaondoka katika mji wa Jericho, vipofu wawili walikuwa wamekaa njiani. Waliposikia Yesu anapita, walimuita kwa kelele, wakisema “**ee mwana wa Daudi tuhurumie.**” Watu waliokuwa karibu walikasirika na wakawaambia wale vipofu wanyamaze kumuita Yesu, lakini wale vipofu walipinga na waliendelea kumuita Yesu tena kwa sauti kubwa zaidi. Yesu alisimama na kuwaita na kuwauliza “mnasemaje?” Wale vipofu waka jibu “**ee Bwana tunataka kuona**”. Yesu aliwahurumia na akawagusa macho yao. Mara wakarudia kuona na wakaanza kumfuata Yesu.

